# SHERIA YA KUREKEBISHA SHERIA YA CHUO CHA UTAWALA WA UMMA, NAM. 1 YA MWAKA 2007 NA MAMBO MENGINE YANAYOHUSIANA NA HAYO

---

## MPANGILIO WA VIFUNGU


**VIFUNGU** **MAELEZO**

**SEHEMU YA KWANZA**
**MASHARTI YA AWALI**

1. Jina fupi na kuanza kutumika.
2. Kusomwa.

**SEHEMU YA PILI**
**VIFUNGU VYA MAREKEBISHO**

3. Marekebisho ya kifungu cha 2.
4. Marekebisho ya kifungu cha 4.
5. Marekebisho ya kifungu cha 5.
6. Kuongezwa vifungu vipya vya 5A na 5B.
7. Kufutwa na kuwekwa badala yake kifungu kipya cha 9.
8. Kufutwa na kuwekwa badala yake kifungu kipya cha 10.
9. Kufutwa na kuwekwa badala yake kifungu kipya cha 11.
10. Marekebisho ya kifungu cha 12.
11. Kufutwa na kuwekwa badala yake kifungu kipya cha 14.

**SHERIA NAM. 9 YA 2022**

**NIMESAINI**

**{DKT. HUSSEIN ALI MWINYI}**
**RAIS WA ZANZIBAR NA MWENYEKITI**
**WA BARAZA LA MAPINDUZI**

**....22 Disemba......, 2022**

# SHERIA YA KUREKEBISHA SHERIA YA CHUO CHA UTAWALA WA UMMA, NAM. 1 YA MWAKA 2007 NA MAMBO MENGINE YANAYOHUSIANA NA HAYO

---

**IMETUNGWA** na Baraza la Wawakilishi, Zanzibar.

## SEHEMU YA KWANZA
## MASHARTI YA AWALI

Jina fupi na kuanza kutumika.

**1.** Sheria hii itajulikana kama Sheria ya Chuo cha Utawala wa Umma (Marekebisho), 2022 na itaanza kutumika baada ya kutiwa saini na Rais na kutangazwa katika Gazeti.

Kusomwa.

**2.** Sheria hii itasomwa pamoja na Sheria ya Chuo cha Utawala wa Umma, Nam. 1 ya Mwaka 2007 ambayo katika Sheria hii itajulikana kama "Sheria Mama".

## SEHEMU YA PILI
## VIFUNGU VYA MAREKEBISHO

Marekebisho ya kifungu cha 2.

**3.** Kifungu cha 2 cha Sheria Mama kinarekebishwa kwa:

(a) kufuta ufafanuzi wa neno "Mkurugenzi" na kuweka badala yake ufafanuzi wa neno "Mkuu wa Chuo" kama ifuatavyo:

"Mkuu wa Chuo" maana yake ni Mkuu wa Chuo aliyeteuliwa kwa mujibu wa masharti ya kifungu cha 9 cha Sheria hii;

(b) kufuta ufafanuzi wa neno "Mrajis".

Marekebisho ya kifungu cha 4.

**4.** Kifungu cha 4(1) cha Sheria Mama kinarekebishwa kwa:

(a) kuongeza aya mpya za (i) na (j) mara baada ya aya (h) kama ifuatavyo:

"(i) kukuza ufanisi wa watumishi wa serikali na binafsi pamoja na kuwaandaa kitaaluma na kiutendaji katika kutekeleza majukumu;

(j) kuimarisha juhudi za mageuzi ya utumishi serikalini na maendeleo katika utumishi wa umma";

(b) kuipa nambari upya aya (i) kuwa aya (k).

Marekebisho ya kifungu cha 5.

**5.** Kifungu cha 5 cha Sheria Mama kinarekebishwa kwa:

(a) kufutwa kifungu kidogo cha (1) na kuweka badala yake kifungu kidogo kipya cha (1) kama ifuatavyo:

"(1) Kutakuwa na Baraza la Chuo ambalo litajumuisha:

(a) Mwenyekiti ambaye atateuliwa na Rais;

(b) Mkuu wa Chuo;

(c) Naibu Mkuu wa Chuo Taaluma, Utafiti na Ushauri;

(d) Naibu Mkuu wa Chuo Utawala, Mipango na Fedha;

(e) Mkurugenzi anayehusika na rasilimali watu kutoka Wizara inayohusika na utumishi wa umma ambaye ni mjumbe anayeingia kwa nafasi yake;

(f) Mwakilishi mmoja kutoka Wizara inayohusika na elimu mwenye cheo cha Mkurugenzi;

(g) Rais wa Jumuiya ya Wanafunzi ya Chuo;

(h) Mjumbe mmoja atakayeteuliwa na Waziri mwenye elimu na uzoefu katika utumishi wa umma au usimamizi wa taaluma".

(b) kufutwa maneno "au chama cha wafanyakazi" yaliyopo katika kifungu kidogo cha (2)".

Kuongezwa vifungu vipya vya 5A na 5B.

**6.** Sheria Mama inarekebishwa kwa kuongezwa vifungu vipya vya 5A na 5B mara baada ya kifungu cha 5 kama ifuatavyo:

"Makamu Mwenyekiti.

**5A.** Wajumbe wa Baraza watamteua mjumbe mmoja miongoni mwao kuwa Makamu Mwenyekiti wa Baraza.

Mjumbe mualikwa.

**5B.** Baraza linaweza kumualika mtu yeyote kuhudhuria katika majadiliano ya vikao vyake kama mtaalamu lakini mjumbe mualikwa huyo hatakuwa na haki ya kupiga kura".

Kufutwa na kuwekwa badala yake kifungu kipya cha 9.

**7.** Kifungu cha 9 cha Sheria Mama kinafutwa na kuwekwa badala yake kifungu kipya cha 9 kama ifuatavyo:

"Uteuzi wa Mkuu wa Chuo.

**9.**-(1) Kutakuwa na Mkuu wa Chuo ambaye atateuliwa na Rais baada ya kupokea mapendekezo kutoka kwa Baraza.

(2) Mtu atakuwa na sifa za kuteuliwa kuwa Mkuu wa Chuo ikiwa mtu huyo ana:

(a) Shahada ya Tatu katika fani ya Utumishi wa Umma, Usimamizi wa Rasilimali watu, Sheria, Utawala wa Biashara, Uchumi au fani nyengine yoyote inayolingana kutoka taasisi inayotambulika na Serikali;

(b) uzoefu wa angalau miaka saba katika fani hiyo; na

(c) uadilifu wa hali ya juu.

(3) Mkuu wa Chuo aliyeteuliwa chini ya masharti ya kifungu kidogo cha (1) cha kifungu hiki, atakuwa ni Afisa Mtendaji Mkuu wa Chuo".

Kufutwa na kuwekwa badala yake kifungu kipya cha 10.

**8.** Kifungu cha 10 cha Sheria Mama kinafutwa na kuwekwa badala yake kifungu kipya cha 10 kama ifuatavyo:

"Kuteuliwa kwa Naibu Wakuu.

**10.**-(1) Kutakuwa na Naibu Mkuu wa Chuo Utawala, Mipango na Fedha na Naibu Mkuu wa Chuo Taaluma, Utafiti na Ushauri Elekezi ambao watateuliwa na Rais.

(2) Naibu Mkuu wa Chuo Utawala, Mipango na Fedha na Naibu Mkuu wa Chuo Taaluma, Utafiti na Ushauri Elekezi watateuliwa kwa njia ya ushindani wa kuajiri kwa mujibu wa masharti kama Rais atakavyoamua.

(3) Mtu atakuwa na sifa ya kuteuliwa kuwa Naibu Mkuu wa Chuo Utawala, Mipango na Fedha ikiwa mtu huyo ana:

(a) Shahada ya Tatu katika fani ya Utumishi wa Umma, Usimamizi wa Rasilimali watu au fani yoyote inayolingana kutoka taasisi inayotambulika na Serikali; na

(b) uzoefu katika Utawala kwa muda usiopungua miaka mitano.

(4) Naibu Mkuu wa Chuo Utawala, Mipango na Fedha:

(a) atakuwa msaidizi mkuu na mshauri mkuu wa Mkuu wa Chuo katika mambo yote yanayohusiana na utawala, mipango na fedha ya Chuo;

(b) atasimamia utekelezaji wa Mpango Mkakati wa Chuo pamoja na miongozo inayotolewa na Chuo;

(c) atasimamia na kuwa kiungo cha idara zilizo chini yake; na

(d) atasimamia mambo yote yanayohusiana na utawala kama itakavyoagizwa na Baraza au Mkuu wa Chuo.

(5) Mtu atakuwa na sifa ya kuteuliwa kuwa Naibu Mkuu wa Chuo Taaluma, Utafiti na Ushauri Elekezi ikiwa mtu huyo ana:

(a) Shahada ya Tatu katika fani ya ualimu, Utumishi wa Umma, Sheria, Usimamizi wa Rasilimali watu au fani yoyote inayolingana kutoka taasisi inayotambulika na Serikali; na

(b) uzoefu katika mambo ya taaluma au utawala kwa muda usiopungua miaka mitano.

(6) Naibu Mkuu wa Chuo Taaluma, Utafiti na Ushauri Elekezi:

(a) atamshauri Mkuu wa Chuo juu ya taaluma na mambo ya kitaalamu ya Chuo;

(b) atawasilisha matokeo ya mitihani kwenye Kamati ya Taaluma na kuyawasilisha katika Baraza la Chuo;

(c) atasimamia utekelezaji wa miongozo yote ya kitaaluma inayotolewa na Chuo na vyombo vya usimamizi; na

(d) atafanya kazi nyengine yoyote kama itakavyoelekezwa na Baraza au Mkuu wa Chuo.

(7) Naibu Mkuu wa Chuo Utawala, Mipango na Fedha na Naibu Mkuu wa Chuo Taaluma, Utafiti na Ushauri Elekezi watashika nafasi kwa kipindi cha miaka mitatu na wanaweza kuteuliwa tena kwa kipindi chengine".

Kufutwa na kuwekwa badala yake kifungu kipya cha 11.

**9.** Kifungu cha 11 cha Sheria Mama kinafutwa na kuwekwa badala yake kifungu kipya cha 11 kama ifuatavyo:

"Idara za Chuo.

**11.**- (1) Chuo kitajumuisha idara kama Baraza litakavyoamua.

(2) Baraza litateuwa Wakuu wa idara za Chuo kutokana na mapendekezo ya Mkuu wa Chuo kwa kuzingatia masharti ya Sheria ya Utumishi wa Umma.

(3) Mtu atakuwa na sifa ya kuteuliwa kuwa mkuu wa idara ikiwa mtu huyo ana:

(a) angalau Shahada ya Pili katika fani ya elimu, biashara, utumishi wa umma, sheria, uchumi au fani yoyote inayolingana kutoka taasisi inayotambulika na Serikali; na

(b) uzoefu wa kazi wa miaka mitano katika taasisi ya kitaaluma.

(4) Wakuu wa idara watashika nafasi kwa kipindi cha miaka mitatu na wanaweza kuteuliwa tena kwa kipindi chengine.

(5) Kazi za wakuu wa idara zitakuwa:

(a) kumsaidia na kumshauri Mkuu wa Chuo na Wasaidizi Wakuu wa Chuo; na

(b) kusimamia mambo yote yanayohusiana na idara".

Marekebisho ya kifungu cha 12.

**10.** Kifungu cha 12 cha Sheria Mama kinarekebishwa kwa kufutwa neno "washiriki wa mafunzo" na kuwekwa badala yake neno "wanafunzi" na marekebisho haya yatafanyika popote ambapo neno "washiriki wa mafunzo au mshiriki wa mafunzo", kama itakavyokuwa, limejitokeza katika Sheria Mama.

Kufutwa na kuwekwa badala yake kifungu kipya cha 14.

**11.** Kifungu cha 14 cha Sheria Mama kinafutwa na kuwekwa badala yake kifungu kipya cha 14 kama ifuatavyo:

"Bajeti ya mwaka.

**14.**-(1) Kwa mujibu wa masharti ya Sheria ya Usimamizi wa Fedha za Umma, Mkuu wa Chuo ataandaa au kusababisha kuandaliwa makisio ya mwaka ya mapato na matumizi ya Chuo kwa mwaka wa fedha husika.

(2) Baraza, kabla ya kuanza kwa mwaka wa fedha, litazingatia na kuidhinisha, kwa kuzingatia mabadiliko na marekebisho kama litakavyoona inafaa makisio yaliyotayarishwa kwa mujibu wa masharti ya kifungu kidogo cha (1) cha kifungu hiki".

Marekebisho ya kifungu cha 16.

**12.** Kifungu cha 16 cha Sheria Mama kinarekebishwa kwa kufutwa maneno "Sheria ya Kuanzishwa kwa Mkaguzi Mkuu Nam. 11 ya mwaka 2003" na kuweka badala yake maneno "Sheria ya Kuanzishwa Ofisi ya Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali".

**UMEPITISHWA** na Baraza la Wawakilishi la Zanzibar, tarehe 12 Disemba, 2022.

..............................................

(RAYA ISSA MSELLEM)

***Katibu wa Baraza la Wawakilishi la Zanzibar.***